

SwahiliWeb

ELECTRONIC DEPOSITORY AND RESOURCE ARCHIVE

www.swahiliweb.net

Archive: Pat Caplan

Document: Mwaharusi Binti Nyihaji

File reference: SW/PC/13015

This document has been downloaded from the SwahiliWeb archive on the understanding that it is copyright under the laws of the United Kingdom and the Berne Convention, and that no further copying, storage or distribution, in any form or by any means, including electronically, is permitted except under the provisions of fair dealing.

Copyright of all materials deposited with SwahiliWeb remains with the copyright holder. Those seeking copyright and associated permissions will be referred to the copyright holder.

**Mwaharusi Binti Nyihaji interview 1985 Kanga village,
transcribed Dec. 2010 by Joseph Bwathondi**

Mwaharusi had become a good friend and important informant on women's affairs at the time of my first visit, when she helped me with understanding the girls' puberty ceremony, and also interpreting women's songs. She had been interviewed for the BBC TV film in 1976, but unfortunately the transcription has been lost. The final interview with her was in 1994 (qv) shortly before her death.

BN: Mimi mlinzi nyumbani naenda tuende wote naye anasema mie sikuchui wewe mshamba

PC: Ah! Anakwambia hivi wewe

BN: Ndio nikaamua kurudi hapa nyumbani kwetu nikaa kaa hapa lakini hakakataa kuniacha ye ye akasema atakuja kunichukua. Mie nikarudi hapa nikaenda kwa wazee wake mie nikawaeleza mie kurudi tena kuishi na Bakari hapana. Baba yake akasema je tumuite ili tuulize? Nikamwambia mimi sitaki. Kitu ninachotaka tu ni kumwambia huyu Bakari anipe talaka yangu tu basi. Pia nikawaeleza wazee Baba mkubwa mzee Jafari huko Kirongwe akenda kwenye mradi wa mbu pale bomani Kilindoni akapiga simu. Bakari amekataa kutoa talaka.

PC: Hivyo.

BN: Sasa ameoaa tena

PC: Wakati huo ulikuwa mwalimu?

BN: Ndio

PC: Na huyu (mtoto) baba yake amekaa naye kidogo

BN: Kakaa nae sana tu. Amemchuka mtoto mdogo wa miaka mine

PC: Nawe ulikubali au ulilazimishwa??

BN: Nililazimishwa

PC: Hukutaka?

BN: Sikutaka.

PC: Sababu ya kurudi hapa ni nini?

BN: Huyu tu mwenyewe alikuwa na hamu ya kumuona mama yake na maisha yalikuwa magumu manake baba yake ni mtu wa kusafiri hapa na hapa na mama aliye kuwa anaishi nae alikuwa mama wa Kambo na siku nyingine alishindia njaa tu bila kula. Sasa ye ye mwenyewe akili yake ikafikiria na baada ya kuona picha ya mama yake akaanza kuijuliza mama yupo wapi na kwa nini hasimtafute? Manake alikuwa anasikia mara mama yake yupo Mafia mara mama yake yupo hivi. Sasa karudi mpaka Dar es salaam, pale Dar es salaam akakutana na jamaa zake . Alifika mwezi wa tisa na hapa Mafia alifika mwezi wa kumi na moja. Akakaa hapa kwa miezi minne mpaka tukasafiri kuja hapa. Mpaka sasa tupo naye.

PC: Sasa atakaa hapa daima ama atarudi pale pale

BN: Mmh! Mie mpaka sasa hatujajua manake hatuja pata habari yoyote toka kwa baba yake.

PC: Sasa yeye anataka kukaa hapa au anataka kurudi?

BN: Yeye anataka kukaa hapa

PC: Sasa anasoma shule hapa ?

BN : Ndio

PC: Darasa la ngapi

BN: Anasoma shule darasa la tano na matokeo yake alikuwa wa 2. Kidogo anapenda kusoma

PC: Hivyo? Lakini namna gani mila inasema mtu anapomuacha mke wake

BN: Kutokana na wazee wanafuata zile sheria zazilizowekwa na wazee wa zamani wanasema hivi mtoto sio wa mke ni wa mume.

PC: Mtoto yoyote sio wa kike sio wa kiume?

BN: Mtoto wa kiume au wa kike wote ni watoto wa mume , kama mkiachana na mke akamkataa mume, mume atawachukua watoto wote lakini kama mume ndio amekataa nitawachukua mimi watoto wote na kuwalea mpaka watakapokuwa wakubwa wataamuya wenyewe waelekee upande gani. Sasa kwa kuwa mimi nilimkataa yeye sasa hasira zake aliamua kuninyan'ganya watoto. Mimi nilijaribu kukataa huku lakini wazee wakasema nimpe

PC: Wakati huu ulishapata mtoto mwengine?

BN: Bado na alikuwa hajao.

PC: Wewe ulikuwa haujapata mtoto mwengine?

BN: Bado nilikuwa hata sina mimba

PC: Katika hawa mkubwa huyu?

BN: Mkubwa huyu ila wamekuwa pamoja.

PC: Ukaendelea na kazi?

BN: Mimi?

PC: Mmh!

BN: Niende nikauchukue ulenije niupikiche niuchemshe nikaanike kwenye juu, unakauka ninakaanga mpunga tunapika bakwe. Bakwe unajua?

PC: Bakwe unakula saa ngapi?

BN: Saa Sita. Kabla ya kwenda kulala, nikienda kulala tena basi.

PC: Leo mwezi 21 au 22

BN: 21 bado siku tisa au nane

PC: Mnategemea mwezi.

BN: Mm. Sikukuu halafu tunafunga tena siku sita

PC: Manafunga tena ?

BN: Ndio. Tukimaliza ile mwezi saba wanaenda karibuni. Lakini mimi siendi.

PC: Lakini huyu bwana atakubali uzae tena?

BN: Sijuhi?

PC: Mmeshazungumza au bado?

BN: Tumeshazungumza

PC: Anasemaje

BN: Nilimwambia tumzike. Mwaka mmoja miwili mpaka mitano. Akaniambia mitano yote? Nikamwambia mitani sio mingi. Lakini ye ye alipenda tupumzike miaka mitatu.

PC: Sasa ye ye amekubali?

BN: Ndio. Sie tukipumzika miaka mitatu halafu tutafuta mtoto

PC: Sasa utafanya nini utakwenda Kilindoni.

BN: Kuchukua dawa, hapa wataleta dawa.

PC: Na Mkunga

BN: Ndio

PC: Za majira

BN: Ndio

PC: Zingine hazipatikani?

BN: Ndio hazipatikani. Wanasema wataleta zile za vidonge vile wanahitaje tena?

PC: Kila siku unakula moja moja?

BN: Ndio Wameandika Family Planning. Kwa hiyo kila siku nakula kidonge kimoja either usiku au asubuhi. Lakini si bora kila usiku.

PC: Saa yoyote ile lakini unatakiwa uile muda ule ule kila siku bila kukosa na ukikosa basi utapata mimba.

BN: Sasa wanasema kama umesahau siku ya pili unakula mbili inasaidia?

PC: Pengine ukikosa siku moja basi lakini ukikosa siku mbili tatu.

BN: Mimi sijawahi kutumia hizi

PC: Haujawahi kutumia. wengine wakitumia wanapoteza maziwa kabisa wengine kichwa kinauma na wengine hawapati shida yoyote.

BN: Mimi hamna lolote. Lakini katika kuziacha nilicha kienyeji. Manake nilishindwa kwenda kuzifata Kilindoni nikasema basi. Sasa nilipokuja kubeba mimba zikawa zinatoka mpaka zikafikia tatu.

PC: Hivyo

BN: Mpaka nilivyokwenda kiliniki nikaweleteza chanzo hasa nilikwa natumia vidonge vya majira, wakanilizia je ulipoacha ulifanya nini? Mie nikawaambia nilivyoacha nikaacha. Wao wakanieleza pindi ukiamua kuacha lazima uwaeleze ndio wakupe dawa zingine au wakupatie sindano kabla ya kutafuta mtoto mwingine. Kwa kasi yako itabidi tukupe dawa za kutumia na upumzike kwa mwaka mmoja. Manake mimba zinapoaribika zinalegeza mji wa uzazi. Sasa kitika kutumia vidogo nimetumia miezi mitatu halafu kukawa hakuna tena vidonge ikabidi nirudi Kilindoni ili nipate matibabu zaidi nao wakaniveke Loop (kitanzi) kwa bahati mbaya hawakuweka vizuri kikatoka nikapeleka tena, wakanambia nikakae mwezi mmoja utakapoona damu yako ya mwezi urudi hapa sasa nikakataa tena sikurudi . sasa vile vyeti ninavyo , vile vipimo ninavyo sasa ilivyotokea hapa imekuwa rahisi kwa mimi kwenda na vipimo na maelezo yote nao wakaaidi kwamba watakapoleta dawa watanichulia na mimi. Sasa sijuhi wataleta lini.

PC: Watakuja leo nafikiri

BN: Watakuja leo?

PC: Pengine. Huyu mama Mkunda amefiwa na Babu yake nimesikia

BN: amefiwa na babu yake? Yupi ?Manake kama amefiwa Yule mama basi na Mohamedi nae atakuwa amefikwa na msiba manake mkewe wa Mohamedi na shangazi yake na huyu mama. Umesikia amekufa lini?

PC: Juzi

BN: Sasa alikuwa amekwenda kuhani msiba

PC: Nadhania alikwenda tu katika matembezi na mzee huyu akafa ye ye akiwa huko. Manake kabla ya kwenda huko tuliongea naye sana na nikawa namuuliza akasema nakwenda zangu kupumzika. Hakuniambia kwamba anakwenda kuhani au amepata msiba. Pengine inawezekana na hakutaka kusema kwamba amapata msiba. Sijuhi. Aminiambia huyu bwana Mganga/Afya.

BN: Naona misiba imekuwa mingi kutokana na homa za kuharisha na kutapika manake watu wanaugua kwa muda mfupi na wanapoteza maisha kama kuna mtoto huyu wa jirani yaani yapata kama masaa kata ya sita mpaka nane toka kuanza kuarisha na kutapika mpaka mauti kumkuta. Walimpeka hospitali lakini kuna kauzembe kalifanyika kidogo na mtoto akapoteza maisha.

PC: Lakini wanasema kama mtoto anapoharisha na kutapika si bora umtengenezee maji ya chumvi na sukari ili kurudisha maji mwilini

BN: Nimesikia, halafu wanasema tena maji ya madafu. Lakini nasikia haya maji yanaonezeka mwilini tu nasikia

PC: Unacheka nini wewe?